

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

MKOA WA RUKWA
Anuani ya Simu: "REGCOM"
Simu Na: 025-2802318/2802137
Nukushi. (025) 2802217
Barua pepe: ras@rukwa.go.tz



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
1 Barabara ya Mkoani,
S.L.P. 128,
55180 Sumbawanga,
RUKWA.

TAARIFA KWA UMMA

**TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TSH BILIONI 1.6 ZA UJENZI WA
MADARAJA NA KALVATI KUPITIA MRADI WA UONDOAJI WA VIKWAZO YA
MIUNDOBINU (BOTTLENECK REMOVAL)**

Wakala wa barabara Mjini na Vijijini (TARURA) Mkoa wa Rukwa unatoa taarifa ya mapokezi ya fedha kiasi cha Tsh 1,678,044,000 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa barabara, madaraja na Kalvati ikiwa ni utekelezaji wa mpango wa kuondoa vikwazo katika maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo.

Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huo zimegawanywa katika Halmashauri tatu kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

NA	JINA LA HALMASHAURI	JINA LA BARABARA	FEDHA ZILIZOTENGWA
1	Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi	Mongamkulu- Korongwe	605,775,000/=
2	Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo	Kanyalakata- Mao- Mkowe	722,000,000/=
3	Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga	Laela- Kavifuti- Miangalua	350,269,000/=
Jumla Kuu			1,678,044,000/=

Katika utekelezaji wa mpango huo madaraja yenye ubora na imara yatajengwa kwa gharama nafuu kwa kutumia mawe ambayo yamethibitishwa kuhimiri kwa maeneo yenye maji mengi.

Imetolewa na

Khadija Dalasia

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Mkoa wa Rukwa

09 Mei 2023

